SOMO LA UBATIZO

**UBATIZO NI NINI**?

Neno ubatizo limetokana na neno la **KIYUNANI BAPTIZO** ambalo lilitafsiriwa kwa lugha ya Kingereza **Baptizing** ambapo kwa Kiswahili ni **Ubatizo.** Maana ya neno **Baptizo** ni **kutosa** au **kuzamishwa** ndani ya maji. Huo ndio ubatizo wa **Kibiblia** na siyo vinginevyo. Ipo mifano mbalimbali katika maandiko matakatifu yanayosadifu ubatizo wa maji mengi:

a. Yohana Mbatizaji (**Math 3:5-6**)
b. Ubatizo wa kule Salim (**Yoh 3:22-23**)
c. Kubatizwa kwa Yesu Kristo (**Mk 1:9-10**), yeye ndiye kielelezo chetu cha kufuata (**1Pet 2:21**)
d. Towashi wa Kushi (**Mdo 8:36-39**)

Mtu anapata wokovu baada ya kumkiri Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wake na kwamba alikufa na akafufuka katika wafu (**Rm 9:10**), hivyo ubatizo wa kuzamishwa katika maji ni **kielelezo cha kukiri** kifo, kuzikwa pamoja na kufufuka na Yesu Kristo **(Rm 6:3-4, Kol 2:12**). Kwa hiyo ili tushiriki kwa imani kifo, kuzikwa na ufufuo wa Kristo katika ubatizo ni lazima tuzame katika maji. Wakati tunapofufuliwa kutoka katika maji, ni ishara kuwa tumefufuliwa kwenye **maisha mapya katika Yesu Kristo, tumezaliwa katika familia ya Mungu wetu mwenye upendo katika upya wa utakatifu**. Ubatizo wa maji pia unaonyesha **utakaso wa kiroho** tunaopata tunapookolewa; kama vile maji husafisha mwili, hivyo Roho Mtakatifu hutakasa mioyo yetu tunapomwamini Yesu Kristo na hivyo tunakuwa tumezaliwa upya katika maisha mapya ya utakatifu.

**ANAYEOSTAHILI KUBATIZWA**

Mtu anayestahili kubatizwa ni lazima atimize mambo yote hapa chini**:**

i. **Toba**: Ni yule aliyetubu dhambi zake (**Mdo 2:37-41)**
ii. **Imani**: Ni yule aliyempokea (kumwamini) Yesu kuwa Bwana na mwokozi maishani mwake **(Mdo 8:37-39, 16:31-33)**
iii. **Uamzi binafsi**: Awe na umri wa kutosha kufanya uamzi wake binafsi wa kumfuata Yesu Kristo. Maandiko matakatifu yanasema aaminiye na kubatizwa ataokoka; hivyo anayemwamini Yesu Kristo ni mtu anayetambua anachokifanya (**Mk 16:16a**).Vitu vyote hivi vinaweza kufanywa na mtu anayejitambua na kwa sababu hizo mtoto hasitahili kubatizwa.

**MIFANO MBALIMBALI YA UBATIZO**:

1. Siku ya Pentekoste , **Mdo 2:37-41**
2. Wakristo wa kule Samaria, **Mdo 8:12**
3. Sauli wa Tarso, **Mdo 9:17-18**
4. Kornelio na nyumba yake, **Mdo 10:47-48**
5. Wakorintho, **Mdo 18:8**
6. Kule Efeso, **Mdo 19:1-5**

**TUBATIZWE WAPI?**

Mahali popote palipo na maji ya kutosha kuzama (**Yoh 3:22-23**), yaweza kuwa kwenye Kisima, Bahari, Ziwa, Mto n.k

**JE, UBATIZO UNAONDOA DHAMBI?**

**Jibu ni hapana.** Damu ya Yesu Kristo pekee ndiyo huondoa na kusafisha dhambi **(1Yoh 1:9). H**ivyo, mtu atapata ondoleo la dhambi zake kwa kutubu na kumpokea Yesu Kristo kuwa Bwana na mwokozi wa maisha yake. Hii ni kusema kwamba mtu aliyeacha dhambi ndiye astahiliye kubatizwa na siyo kwamba mtu abatizwe ili kusafisha dhambi zake.

**KWA NINI TUBATIZWE?**

1. Ni kutimiza haki yote **(Mt 3:13-16; Lk 7:29-30),** yaani maagizo yote **(Zab 119:6, 172)**
2. Kufuata mfano wa Yesu Kristo mwanzilishi wa Imani yetu (**Mk 1:9-10**)
3. Kutii agizo la Yesu Kristo (**Mt 28: 19-20**).
4. Ili kushuhudia ulimwengu kwa nje yale yalitokea ndani ya mioyo yetu (**Rm 10:9**) – kwamba katika dhambi mimi nimekufa, nimezikwa na kufufuka naYesu Kristo (**Rm 6:3-4, Kol2:12**). Kwamba moyo wangu umesafishwa na kuwa mpya katika Kristo Yesu.
5. Ili kuonesha kuukubali mpango wa Mungu – (**LK 7:29-30)**

**JE, WATOTO WADOGO WANASTAHILI KUBATIZWA?**

**Jibu ni hapana,** hii ni kama ilivyoelezwa hapo juu kwamba ubatizo unaambatana na imani**.** Tunajifunza kutoka kwa **Bwana** Yesu Kristo mwenyewe ambaye ndiye kielelezo au mfano wa jinsi tunavyotakiwa kuishi na kutenda **(1PETRO 2:21; 1WAKORITHO 11;1**), alivyowabariki watoto bila kuwabatiza (**Mk 10:13-15)**.

Watoto wadogo wanabarikiwa tu na siyo kuwabatiza kwa sababu hawajui kupambanua kati ya mema na mabaya (**WAEBRANIA 5;13-14**). Ubatizo unafanya kwa mtu baada ya kulisikia Neno la Mungu na kuamini Kristo kisha kutubu dhambi zake zote. Lazima mtu asafishwe dhambi zake kwanza kwa damu ya Yesu Kristo kwa njia ya imani. Yesu Kristo mwenyewe alibarikiwa akiwa mtoto mdogo na kubatizwa alipokuwa mtu mzima (**Lk 2:27,34; Lk 3:21-23**).

**JE, NAWEZA KUBATIZWA ZAIDI YA MARA MOJA?**

Ubatizo wa kibiblia unafanywa kwa mtu mara moja tu kama ambavyo Yesu Kristo alizikwa mara moja na kufufuka mara moja tu. Kama mtu alibatizwa bila kutubu dhambi zake na kumpokea Yesu Kristo moyoni mwake, huo haukuwa ubatizo wa kibiblia ni sawa na mtu aliyeenda kuoga maji. Kama mtu alibatizwa utotoni anahitaji kukiri kumpokea Yesu Kristo maishani mwake na kutubu dhambi zake mwenyewe ndipo ataweza kubatizwa kibiblia. Mtu akirudi nyuma kiroho, akirejea na kutubu hatakiwi kubatizwa tena. Kama mtu alinyunyiziwa maji kichwani au usoni hakubatizwa kibiblia, ni lazima azamishwe katika maji ndipo atakuwa ameshiriki mauti ya Yesu Kristo kwa njia ya ubatizo (**Kol 2:12, Rm 6:4-5**).

Wapo watu ambao walibatizwa mara mbili katika biblia ingawa mwanzo walibatizwa katika maji tele (**MATENDO 19:3-5**). Iwapo mwanzoni mtu alibatizwa kwa ubatizo usio wa kibiblia, anapaswa kubatizwa ubatizo wa kibiblia kama Yesu alivyosema tujifunze kwake **(MATHAYO 11:29**).

**JE, LAZIMA KUBADILISHA JINA WAKATI WA KUBATIZWA?**

**Jibu ni hapana**. Siyo lazima ubadili jina lako isipokuwa pale jina lako linapokuwa na ushuhuda mbaya kwa jamii inayokuzunguka (**2 WAKORINTHO 3:2-3** ). Sauli baada ya kuokoka alibadili jina lake akawa Paulo kutokana na ushuhuda mbaya wa jina la Sauli. Unapobadili jina kwa ajili ya ubatizo, badili jina lako tu siyo jina la baba yako kwani wewe ndiye uyemwamini Yesu Kristo.